



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. Na. DED/NMT/C.50/7/448

21 Desemba, 2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI (LINARUDIWA)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kupitia Kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA.170/367/01 "TEMP"/46 cha tarehe 7 Oktoba, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Anatangaza nafasi ya kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa kujaza nafasi ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (Nafasi 1)**

(a) Sifa za Mwombaji:

- Awe amehitimu Kidato cha nne au sita na cheti cha mafunzo (**NTA LEVEL 5**) katika fani mojawapo kati ya hizi; - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology). Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(b) Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja III

Mtendaji wa Kijiji atatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na Mali zao,
- Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji,
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo kijijini,
- Katibu wa Mikutano Mkuu na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji,
- kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika ngazi ya Kijiji.

(c) Ngazi ya Mshahara:

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

(d) Masharti ya Jumla


- (i) Maombi yote yatumwe na nakala za vyeti vya taaluma, utaalamu na cheti cha kuzaliwa, nakala ya vyeti husika vithibitishwe na mahakama au na mtu yeyote aliyeidhinishwa na Serikali.
- (ii) Testimonials' 'Provisionals Results', Statement of Results; Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA**.
- (iii) Barua za maombi ziambatane na nakala ya kitambulisho cha Utaifa au namba ya Kitambulisho cha Utaifa (NIDA)
- (iv) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kuwa vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika ya TCU na NECTA.
- (v) Watumishi wote waliowahi kufanya kazi katika katika Utumishi wa Umma wakaacha, wakastaafu, wakastaafishwa au kufukuzwa hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- (vi) Vyeti vyote vitafanyiwa uhakikikwa kushirikiana na mamlaka husika za NECTA na TCU na vyuo waombaji walivyosomea na endapo itagundulika mwombaji amehusisha vyeti vya kughushi kwenye maombi yake atachukua hatua za kisheria
- (vii) Mwombaji ambatishe Picha mbili za rangi (Passport Size) za hivi karibuni,
- (viii) Maombi yaambatishwe na maelezo binafsi (CV),
- (ix) Mwombaji awe na umri wa miaka 18 hadi 45
- (x) Waombaji walioomba mara ya kwanza waombe upya


Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifutayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya Namtumbo,
S. L. P 55,
NAMTUMBO.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 03/01/2022 saa tisa Alasiri.

NB: Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.natumbodc.go.tz


Ambokile Paul
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
NAMTUMBO



Mkurugenzi Mtendaji (W) S. L. P 55, Namtumbo Mkoa wa Ruvuma, Simu +255 252675008,
Nukushi +255 25 2675008, Barua pepe ded@namtumbodc.go.tz